
OFISI YA RAIS

# UTUMISHI

NA UTAWALA BORA






Rais **Mhe. Dkt. Samia Suluhu** Hassan awataka Watumishi wa Umma Kufuata Nyayo za Hayati Moringe Sokoine



TOLEO LA OKTOBA 2024

# 1 RAIS MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN AWATAKA WATUMISHI WA UMMA KUFUATA NYAYO ZA HAYATI MORINGE SOKOINE



*Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa na Viongozi mbalimbali waliohudhuria hafla ya Uzinduzi wa Kitabu cha Hayati Edward Moringe Sokoine kinachohusu Maisha na Uongozi wake.*

*na Lusungu Helela - Dar es Salaam*

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amewataka Watumishi wa Umma kutanguliza mbele uzalendo muda wote wanapokuwa ndani na nje ya utumishi wao huku akisisitiza kuwa Mtumishi wa umma muadilifu ni rahisi sana kuonekana na kutambulika kama ambavyo hivi sasa Waziri Mkuu wa zamani Hayati Edward Moringe Sokoine anatambulika kutokana na uzalendo na uadilifu wake

Rais Mhe. Dkt. Samia ametoa kauli hiyo hivi karibuni wakati wa hafla ya kuzindua Kitabu kinachohusu Maisha na Uongozi wake Hayati Edward Moringe Sokoine kwenye hafla iliyofanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam.

"Hayati Sokoine alikuwa mfano na kiongozi aliyejali uwajibikaji, haki na uwazi. Aliamini katika dhana ya utumishi wa umma akitambua kwamba uongozi ni jukumu la kutumikia wananchi, kwa moyo wa kujitolea, akijenga nidhamu ya utendaji kazi ndani ya serikali, akisisitiza utumishi bora uadilifu na ufanisi katika kila hatua ya maendeleo.

"Leo tunapoangalia historia na mchango wake tunapata somo kubwa namna ya kiongozi wa kweli anavyoweza kuacha alama isiyofutika, juu ya kitabu hiki kizazi cha sasa na baadaye kitajifunza juu na maono na fikra za kiongozi huyu ambaye alikuwa mfano wa kuigwa katika siasa za Tanzania,"

"Niwashukuru familia ya Sokoine, maisha ya ndani kufikishwa kwa kiongozi huyu na wadau wa maendeleo kusoma kitabu hiki kuboresha utendajii wa kazi ili kuleta maendeleo na kufanikisha uchumi wa nchi. Huu ni urithi wa thamani utakaodumu vizazi na vizazi,"



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene akizungumza kabla ya kumkaribisha Rais Mhe.Dkt.Samia Suluhu Hassan kuzungumza na wananchi na viongozi mbalimbali wakati wa uzinduzi wa kitabu cha Edward Moringe Sokoine, Maisha na Uongozi wake.*

Kwa upande wake Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene amesema Waziri Mkuu wa zamani Hayati Edward Moringe Sokoine ameacha alama kubwa katika uongozi wake na atakumbukwa na vizazi hata vizazi kutokana na mambo mbalimbali aliyofanya ikiwemo kujenga nidhamu katika Utumishi wa Umma

Amesema Hayati Sokoine alikuwa ni Kiongozi aliyejali uwajibikaji, uadilifu na ufanisi katika kila hatua ya maendeleo na aliyeongoza kwa maadili mema, maono na aliyezingatia usawa kwa watu wake.


Aidha, Mhe. Simbachawene ametumia fursa hiyo kutoa rai kwa Watumishi wa Umma, Wadau wa Maendeleo pamoja na Watanzania wote kusoma Kitabu cha Maisha na Uongozi wa Hayati Edward Moringe Sokoine ili kupata mafundisho yao wa kazi na hatimaye kuleta maendeleo na kuimarisha ustawi wa Taifa




***Rais Mhe.Dkt.Samia Suluhu Hassan akizungumza na wananchi na viongozi mbalimbali wakati wa uzinduzi wa kitabu cha Edward Moringe Sokoine, Maisha na Uongozi wake***



*Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa kwenye picha ya pamoja na familia ya hayati Edward Moringe Sokoine kabla ya kuzindua Kitabu kinachohusu Maisha na Uongozi wake.*








# 2 WACHEZAJI WA UTUMISHI WAPOKELEWA KISHUJAA, WAZIRI SIMBACHAWENE AONGOZA KUPOKEA VIKOMBE VYA USHINDI

*na Mwandishi Wetu*

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene amewapongeza Viongozi na wanamichezo wa Ofisi yake kwa kupambana na kutwaa vikombe viwili vya ubingwa katika michezo inayosimamiwa na Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali Tanzania (SHIMIWI).

Mhe. Simbachawene ametoa pongezi hizo hivi karibuni wakati wa hafla fupi iliyofanyika katika Jengo la Ofisi za Utumishi, Mtumba jijini Dodoma kwa lengo la kupokea Vikombe vya ushindi katika mchezo wa mpira wa miguu na mashindano ya baiskeli ya SHIMIWI.

"Niwapongeze kwa kuleta heshima kubwa katika Ofisi hii, ubingwa wa mpira wa miguu na ushindi wa nafasi ya kwanza kwenye mashindano ya baiskeli unadhihirisha dhamana yetu ya kusimamamia Watumishi wa Umma na kuwa mfano kwa kila jambo lililo jema" alisema Mhe. Simbachawene.

Amesisitiza kuwa, ushindi wa vikombe viwili ni hatua kubwa lakini kubwa zaidi ni kitendo cha kubeba kombe la mpira wa miguu. Kombe la mpira wa miguu linaleta maana zaidi kuliko waliochukua vikombe vingine.

Aidha, Mhe. Simbachawene ametumia fursa hiyo kumpongeza Katibu Mkuu-UTUMISHI Bw. Juma Mkomi kwa kuwa chachu ya kuimarisha michezo Ofisini amemuomba kuendelea kuwa na ari hiyo ili kujenga afya njema za watumishi mahala pa kazi.

Naye Naibu Waziri Mhe. Sangu amewapongeza wanamichezo hao kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kupambana ili kufikia malengo yaliyokuwa yamewekwa ya kuleta ushindi.

Amesema kuwa, ushindi huo wa vikombe viwili unatokana na jitihada kubwa zilizofanywa na Katibu Mkuu, Bw.Juma Mkomi ya kuwa karibu na wachezaji hao na kuwapa hamasa na zaidi kuwawezesha ipasavyo.

Halikadhalika, ametoa pongezi za kipekee kwa Bw. Mkomi kwa kuwa kiungo muhimu sana kwa watumishi wa Ofisi hiyo, mathalani ukaribu wake kwa wachezaji umekuwa chanzo cha kufanya vizuri kwenye michezo ya SHIMIWI na ameombwa kuendelea kuwa na moyo huo ambao matokeo yake yanaonekana kwa kila mmoja mtumishi.

Naye Katibu Mkuu Mkomi amewapongeza wachezaji hao huku akimshukuru Waziri Mhe. Simbachawene pamoja na Naibu Waziri Mhe. Deus Sangu kwa ushirikiano wao mkubwa walionao katika kupenda na kuthamini michezo.

"Nakushukuru Naibu Waziri Mhe. Sangu kwa kufika katika kambi za mashindano hayo na kutoa hamasa kubwa wa watumishi wetu, hamasa hiyo imeleta ushindi ambao tunafurahia hii leo" alisema Bw. Mkomi

Mashindano ya SHIMIWI yalihitimishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora tarehe Oktoba 5, 2024 Mkoani Morogoro.



*Katibu Mkuu, Bw.Juma Mkomi akipokea kikombe cha mshindi wa kwanza wa mpira wa miguu na kutoka kwa Bw. Charles Shija wakati wa hafla fupi ya mapokezi iliyofanyika jijini Dodoma mara baada ya timu hiyo kunyakua vikombe viwili katika Mashindano ya 38 ya Shirikisho la Michezo la Wizara na Idara za Serikali Tanzania ( SHIMIWI) yaliyofikia Kilele chake hivi karibumi Mkoani Morogoro*





*Katibu Mkuu, Bw.Juma Mkomi akipokea kikombe cha mshindi wa kwanza wa mpira wa miguu na kutoka kwa Bw. Charles Shija wakati wa hafla fupi ya mapokezi iliyofanyika jijini Dodoma mara baada ya timu hiyo kunyakua vikombe viwili katika Mashindano ya 38 ya Shirikisho la Michezo la Wizara na Idara za Serikali Tanzania ( SHIMIWI) yaliyofikia Kilele chake hivi karibumi Mkoani Morogoro*



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene akiwa na Naibu Waziri wa Ofisi hiyo Mhe.Deus Sangu wakipata maelezo kutoka kwa Katibu Mkuu, Bw.Juma Mkomi wakati wa hafla fupi ya kupokea vikombe vya mshindi wa kwanza wa mpira wa miguu pamoja na mshindi wa kwanza wa mbio za baiskeli mara baada ya kunyakua katika Mashindano ya 38 ya Shirikisho la Michezo la Wizara na Idara za Serikali Tanzania ( SHIMIWI) yaliyofikia Kilele chake hivi karibumi Mkoani Morogoro*



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene akipokea kikombe cha mshindi wa kwanza wa mpira wa miguu kutoka kwa na Bw. Charles Shija huku akishuhudiwa na Naibu Waziri wa Ofisi hiyo Mhe.Deus Sangu (kulia) pamoja na Katibu Mkuu, Bw.Juma Mkomi (kushoto) wakati wa hafla fupi ya mapokezi iliyofanyika jijini Dodoma mara baada ya kunyakua vikombe viwili katika Mashindano ya 38 ya Shirikisho la Michezo la Wizara na Idara za Serikali Tanzania ( SHIMIWI) yaliyofikia Kilele chake hivi karibumi Mkoani Morogoro*

# 3 NAIBU WAZIRI SANGU: MAAMUZI YA MAMLAKA ZA AJIRA NA NIDHAMU KWA WATUMISHI ZINAIINGIZIA HASARA SERIKALI



*Baadhi ya Makamishna wakimsiliza Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Deus Sangu mara baada ya kuwasili kwa ajili ya kushiriki kusikiliza rufaa na malalamiko yaliyowasilishwa na watumishi ambao hawakuridhika na uamuzi uliofanywa na Mamlaka zao za Ajira na Nidhamu katika maeneo yao ya kazi*

*na Lusungu Helela - Dar es Salaam*

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Deus Sangu amesema suala la weledi katika kushughulikia mashtaka ya kinidhamu kwa Watumishi wa Umma nchini bado ni ya kiwango cha chini sana, hali inayopelekea Serikali kuingia gharama pindi rufaa na malalamiko ya mtumishi ambaye hakuridhika na uamuzi wa Mamlaka hizo yanaposikilizwa na kutolewa uamuzi na Tume ya Utumishi wa Umma.

Amesema Mamlaka hizo zimekuwa hazitoi fursa ya kujitetea kwa mtumishi mtuhumiwa kabla ya mtumishi huyo kuhukumiwa jambo ambalo ni moja ya misingi ya utoaji haki kwa mujibu wa Katiba ya nchi yetu na Sheria zilizopo.

Mhe. Sangu ametoa kauli hiyo hivi karibuni Mkoani Dodoma mara baada ya kushiriki kusikiliza rufaa na malalamiko ya baadhi ya Watumishi wa Umma ambao hawakuridhika na uamuzi uliofanywa na Mamlaka zao za Ajira na Nidhamu katika maeneo yao ya kazi wakitoa utetezi wao mbele ya Makamishna wa Tume.

Amesema kamati za uchunguzi zinazoundwa zinapaswa kutekeleza wajibu wake ipasavyo ikiwa ni pamoja na kuhakikisha taarifa zao za uchunguzi kubainisha iwapo makosa waliyoshtakiwa nayo watumishi watuhumiwa yamethibitika au kutokuthibitika kutendeka.

Amesema hali hiyo imekuwa ikiiumiza Serikali kwa kuanza kulazimika kulipa mshahara Mtumishi katika kipindi chote alichokuwa amefukuzwa kazi au kusimamishwa.

Amesema mbali na gharama hizo ambazo Serikali hulazimika kuingia, pia katika hatua za mwanzo kabisa pindi Mtumishi anapotuhumiwa kuwa na makosa huanza mchakato wa kuunda kamati za uchunguzi ambazo wajumbe wake hulipwa posho ambayo ni fedha za Serikali.

Kufuatia hatua hiyo, Mhe. Sangu amesema anatamani kuona rufaa na malalamiko yanayopelekwa Tume ya Utumishi wa Umma yamalizika katika ngazi ya chini yakiwa yamefanyika kwa weledi pamoja na idadi yake kupungua ili Tume hiyo iweze kujikita kwenye masuala ya ukaguzi na mafunzo ili kuboresha ufanisi katika Utumishi wa Umma nchini.

Amesema kuwa mashtaka mengi yanayopelekwa Tume hiyo yamebainika kuwa na kasoro za wazi, hivyo kumpa nguvu mtumishi mtuhumiwa kuwasilisha rufaa na malalamiko yake katika Tume ya Utumishi wa Umma.



***JUU:*** *Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Deus Sangu akizungumza leo na Makamishna wa Tume ya Utumishi wa Umma mara baada ya kushiriki kusikiliza rufaa na malalamiko yaliyowasilishwa na watumishi watuhumiwa ambao hawakuridhika na uamuzi uliofanywa na Mamlaka zao za Ajira na Nidhamu katika maeneo yao ya kazi*



***KUSHOTO:*** *Baadhi ya Makamishna wakimsiliza Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Deus Sangu mara baada ya kuwasili kwa ajili ya kushiriki kusikiliza rufaa na malalamiko yaliyowasilishwa na watumishi ambao hawakuridhika na uamuzi uliofanywa na Mamlaka zao za Ajira na Nidhamu katika maeneo yao ya kazi.*



*Mwenyekiti wa Makamishna wa Tume ya Utumishi wa Umma, Mhe. Jaji (Mst.) Hamisa Hamis Kalombola akizungumza mara baada ya Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Deus kuwasili kwa ajili ya kushiriki kusikiliza rufaa na malalamiko yaliyowasilishwa na watumishi ambao hawakuridhika na uamuzi uliofanywa na Mamlaka zao za Ajira na Nidhamu katika maeneo yao ya kazi*



# 4 MHE. SIMBACHAWENE AWATAKA WAAJIRI KUTENGA BAJETI YA WATUMISHI WA UMMA KUSHIRIKI SHIMIWI



*na Lusungu Helela - Morogoro*

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene amewataka Waajiri kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya kuwawezesha Watumishi wa Umma kushiriki Michezo ya SHIMIWI ili kukidhi malengo na misingi ya kuanzishwa kwa michezo hiyo ili kuleta tija iliyokusudiwa

Mhe. Simbachawene ametoa kauli hivi karibuni Mkoani Morogoro wakati akifunga Mashindano ya 38 ya Shirikisho la Michezo la Wizara na Idara za Serikali Tanzania ( SHIMIWI) ambapo amesema michezo hiyo sio hiari bali ni lazima kwa Watumishi wa Umma nchini

Ametumia fursa hiyo kuwataka Makatibu Wakuu pamoja na Makatibu Tawala kuacha kudharau michezo hiyo huku akisisitiza kuwa michezo hiyo ipo kisheria.

Amesema michezo hiyo ni muhimu mbali ya kuimarisha afya kwa watumishi wa umma pia inawasaidia watumishi hao kuondoa msongo wa mawazo.

Kufuatia hatua hiyo Mhe, Simbachawene amewataka Watumishi hao walioshiriki michezo hiyo wakaoneshe utofauti mahali pa kazi ili kuendelea kuipa heshima michezo hiyo ili kuendelea kuwashawishi waajiri wao kutenga bajeti ya ushiriki.

Katika hatua nyingine, Mhe. Simbachawene amewataka Watumishi hao kushiriki uchaguzi wa Serikali za Mitaa ambapo amesema ushiriki wao ni muhimu sana kwa ajili ya mustakabali wa taifa endelevu.

''Watumishi walio wengi wanaona kujiandikisha na kushiriki kupiga kura hususan uchaguzi wa Serikali za Mitaa ni kama kupoteza muda na sio hadhi yao,nawaomba sana mshiriki kwenye uchaguzi huu.Mhe. Simbachawene amesisitiza.

mesema suala la uchaguzi wa viongozi ni jukumu la wananchi wote wakiwemo Watumishi wa Umma

Naye, Mwenyekiti wa SHIMIWI Daniel Mwalusamba amesema jumla ya Watumishi 2995 wameshiriki kwenye michezo hiyo mwaka huu

Aidha, ametumia fursa hiyo kuwashukuru Viongozi mbalimbali waliojitoa kwa hali na mali katika kuhakikisha mashindano hayo yanafanikiwa.



*Katibu Mkuu- UTUMISHI, Bw. Juma Mkomi akizungumza kabla Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe.George Simbachawene kufunga Mashindano ya 38 ya Shirikisho la Michezo la Wizara na Idara za Serikali Tanzania ( SHIMIWI) yaliyofikia Kilele chake hivi karibuni Mjini Morogoro*



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe.George Simbachawene (kushoto) akiwa na Katibu Mkuu- UTUMISHI, Bw. Juma Mkomi (kulia) wakiwa pamoja na Mshindi wa kwanza wa mbio za Baiskeli, Bw. Hassan Ligoneko akiwa ameshikilia kombe mara baada ya kukabidhiwa wakati wa ufungaji wa Mashindano ya 38 ya Shirikisho la Michezo la Wizara na Idara za Serikali Tanzania ( SHIMIWI) yaliyofikia Kilele chake hivi karibuni Mjini Morogoro.*



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe.George Simbachawene akikabidhi zawadi mbalimbli kwa Washindi kabla ya kufunga Mashindano ya 38 ya Shirikisho la Michezo la Wizara na Idara za Serikali Tanzania ( SHIMIWI) yaliyofikia kilele chake hivi karibuni Mjini Morogoro.*




*Mkurugenzi mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao Eng. Benedict Ndomba akizungumza kabla ya kumkaribisha Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe.Deus Sanga kwa ajili ta kufunga mafunzo kwa vitendo kwa Wanafunzi 65 wa Vyuo Vikuu mbalimbali yaliyofanyika kwa kipindi cha muda wa wiki kumi katika Kituo cha Ubunifu na Utafiti cha eGA kilichopo jijini Dodoma*



Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Deus Sangu akizungumza leo mara baada kukagua Mradi wa ujenzi wa ofisi za TAKUKURU Wilaya ya Nzega Mkoani Tabora

# 5 NAIBU WAZIRI SANGU: TAKUKURU IJIPAMBANUE KWA KUTENDA HAKI NA UADILIFU

*na Lusungu Helela - Dar es Salaam*

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Deus Sangu ameitaka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuwa mfano kwa kujipambanua kutenda haki na kuonesha uadilifu katika jamii huku akisisitiza kuwa hatua kali zitachukuliwa kwa Mtumishi yeyote wa TAKUKURU atakayebainika kuwa sio muadilifu

Mhe. Sangu ametoa kauli hiyo hivi karibuni mara baada ya kukagua Mradi wa ujenzi wa ofisi za TAKUKURU Wilaya ya Nzega Mkoani Tabora uliogharimu kiasi cha Sh. Milioni 314.2 hadi kukamilika kwake.

Amesema TAKUKURU ni chombo kinachohitaji watumishi wenye uadilifu wa hali ya juu hivyo kwa Mtumishi yeyote ambaye sio muadilifu TAKUKURU si mahali sahihi kwa yeye kufanya kazi.

Amesema ni jambo lisilokubalika kwa chombo hicho nyeti cha kuzuia rushwa halafu kukawa na Watumishi mabingwa wa kupokea.

Akizungumzia ujenzi wa ofisi hizo, Mhe. Sangu ameipongeza TAKUKURU kwa kuonesha mfano namna fedha za Watanzania zinavyotakiwa kutumika kwani thamani ya fedha iliyotumika kwenye ujenzi wa ofisi hizo unaonekana.

''TAKUKURU ni chombo kinachosimamia uadilifu na kinatakiwa kiwe cha kwanza kuonesha uadilifu kwa matendo yake, kwa namna nilivyokagua jengo hili nimeridhishwa mno naamini wateja wetu watakaokuja hapa kwa ajili ya kuchunguzwa hili jengo litumike kama mfano kwa kuonesha thamani ya fedha iliyotumika, niwapongeze sana kwa jambo kubwa mlilolifanya hapa'' amesisitiza Mhe. Sangu.



Hata hivyo, Mhe. Sangu ameiagiza TAKUKURU kuhakikisha inahamia katika ofisi hizo za kisasa ndani ya mwezi huu ikizingatiwa kuwa ofisi wanazozitumia kwa sasa katika Wilaya hiyo kodi yake ya pango itafikia ukomo mwezi huu.

Amesema kukamilika kwa Ofisi hizo kunaonesha dhamira ya dhati ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuhakikisha TAKUKURU inawajibika ipasavyo kwa wananchi.

Kufuatia hatua hiyo, Mhe. Sangu ametumia fursa hiyo kumshukuru Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maono yake makubwa ya kukubali kutoa fedha hizo ili kuhakikisha Watumishi wa Takukuru katika Wilaya ya Nzega wanatimiza wajibu wao kwa kufanya kazi katika Ofisi za kisasa.

Katika hatua nyingine, Mhe. Sangu ameitaka TAKUKURU kuzifanyia kazi kwa wakati nyaraka za mikataba ya miradi ya maendeleo ambazo huwasilishwa kwao kutoka kwa Wateja wao .

Amesema kama jambo limekamilika au halina uchunguzi wowote ni muhimu nyaraka hizo zikarudishwa haraka kwa wahusika badala ya kukaa nazo kwa kipindi cha muda mrefu kwani lengo la TAKUKURU kupewa nyaraka hizo ni kuzuia rushwa ili kuhakikisha miradi hiyo ya maendeleo inapoanza kutekelezwa isiharibike.

Amesisitiza kuwa ni muhimu kwa nyaraka hizo za mikataba kufanyiwa kazi ipasanyo ili kuhakikisha miradi hiyo ya maendeleo inakamilika kwa viwango vinavyotakiwa kwa kuonesha thamani ya fedha.



*Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Deus Sangu akisalimiana na baadhi ya Watumishi wa TAKUKURU kabla ya kuanza kukagua Mradi wa ujenzi wa ofisi za TAKUKURU Wilaya ya Nzega Mkoani Tabora*




*Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Deus Sangu akiwa kwenye picha ya pamoja na Watumishi wa TAKUKURU mara baada kukagua Mradi wa ujenzi wa ofisi za TAKUKURU Wilaya ya Nzega Mkoani Tabora*




*Muonekano wa sehemu ya nje ya Ofisi za TAKUKURU Wilaya ya Nzega Mkoani Tabora mara baada ya kukamilika kwake*



*Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Deus Sangu akipata maelezo kutoka kwa Kamanda wa TAKUKURU Wilaya ya Nzega, mara baada kukagua Mradi wa ujenzi wa ofisi za TAKUKURU Wilaya ya Nzega Mkoani Tabora*



# 6 KATIBU MKUU MKOMI AWATAKA WADAU KUTOA MAONI YA MFUMO WA TATHMINI YA RASILIMALIWATU ILI KUBORESHA UTENDAJI KAZI KATIKA UTUMISHI WA UMMA

*Na. Veronica Mwafisi - Dodoma*

Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Bw. Juma Mkomi amesema Mfumo wa Tathmini ya Mahitaji ya Rasilimaliwatu utaisaidia Serikali kufanya msawazo katika Utumishi wa Umma ili kuwa na mtawanyo mzuri wa watumishi kwa lengo la kuboresha utendaji katika utumishi wa umma.

Bw. Mkomi ameyasema hayo hivi karibuni jijini Dodoma wakati akifungua kikao kazi cha kujadili matokeo ya tathmini ya mahitaji ya rasilimaliwatu katika utumishi wa umma kwa Wakurugenzi wa Idara za Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu kutoka Wizara zote, wataalamu wanaosimamia uandaaji na ujazaji wa mahitaji ya watumishi kutoka wizara zote pamoja na Wakurugenzi na wataalamu kutoka Ofisi ya Rais-UTUMISHI.

Bw. Mkomi amesema kila Mkurugenzi anafahamu umuhimu wa mahitaji ya rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma na kuwasihi wafanye tathmini ya kutosha.

"Ukisema una watumishi wachache, tutakuuliza unahitaji watumishi wangapi? kwani unatakiwa uwe umefanya tathmini ya kutosha kwasababu inawezekana kumhitaji kwako mtumishi au kutokumhitaji kunatokana na matakwa yako na si mfumo unaokufahamisha kuwa mtumishi huyu ni wa ziada." Bw. Mkomi amesema.

Bw. Mkomi amesema msawazo katika utumishi wa umma unahitajika kufanywa katika maeneo mawili ikiwemo mjini ili kutokuwa na watumishi wa ziada ambao hawana majukumu ya kutosha katika maeneo yao ya kazi lakini pia msawazo huo utasaidia kuunganisha familia.




*Katibu Mkuu- UTUMISHI, Bw. Juma Mkomi akifungua kikao kazi cha Wakurugenzi wa Idara za Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu na Maafisa Utumishi kutoka Serikalini kilicholenga kujadili Matokeo ya Tathmini ya Mahitaji ya Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma jijini Dodoma*



*Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Bw. Juma Mkomi (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya washiriki wa kikao kazi cha Wakurugenzi wa Idara za Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu na Maafisa Utumishi kutoka serikalini mara baada ya kufungua kikao hicho kilicholenga kujadili Matokeo ya Tathmini ya Mahitaji ya Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma jijini Dodoma . Kulia kwake ni Mkurugenzi wa Idara ya Uendelezaji Taasisi, Bw. Nolasco Kipanda.*

Bw. Mkomi ameongeza kuwa, msawazo hautaweza kufanyika bila kuwa na taarifa halisi ya mahitaji na idadi ya watumishi waliopo katika maeneo husika hivyo, ni vizuri washiriki wakaangalia namna ya kufanya kwani inatakiwa kujua watumishi wangapi wanahitajika wapi, wakafanye nini na baada ya kujua hayo itapatikana nafasi nzuri ya kuboresha.

"Niwatake mshiriki kikamilifu kwa kuipokea taarifa hiyo, kuichambua na kutoa mapendekezo yatakayosaidia kuboresha Mfumo huo utakaowezesha kuwa na mtawanyo mzuri wa watumishi katika Taasisi za Umma." Bw. Mkomi amesisitiza.

Awali, Mkurugenzi wa Uendelezaji Taasisi, Bw. Nolasco Kipanda amesema lengo la kikao kazi hicho ni kujadili matokeo ya tathmini ya Rasilimaliwatu katika Taasisi za Umma ili kupata maoni toka kwa wadau hao na kuboresha mfumo huo katika Utumishi wa Umma kwa masilahi mapana ya taifa.

Kikao kazi hicho kitajadili mada mbalimbali ikiwemo Matokeo ya Tathmini ya Mahitaji ya Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma, matokeo ya Wizara na vigezo kwa upande wa Wizara na Makundi ya Taasisi.





*Mkurugenzi wa Idara ya Uendelezaji Taasisi, Bw. Nolasco Kipanda akitoa neno la utangulizi kabla ya kumkaribisha Katibu Mkuu - UTUMISHI, Bw. Juma Mkomi (hayupo pichani) kufungua kikao kazi cha Wakurugenzi wa Idara za Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu na Maafisa Utumishi kutoka serikalini kilicholenga kujadili Matokeo ya Tathmini ya Mahitaji ya Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma jijini Dodoma*




*Mkurugenzi wa Idara ya Uendelezaji Taasisi, Bw. Nolasco Kipanda akitoa neno la utangulizi kabla ya kumkaribisha Katibu Mkuu - UTUMISHI, Bw. Juma Mkomi (hayupo pichani) kufungua kikao kazi cha Wakurugenzi wa Idara za Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu na Maafisa Utumishi kutoka serikalini kilicholenga kujadili Matokeo ya Tathmini ya Mahitaji ya Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma jijini Dodoma*

# 7 OFISI YA RAIS- UTUMISHI: KIMBILIO KWA HUDUMA ZA KIUTUMISHI



Kaimu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Bw. Xavier Daudi amewapongeza watumishi wa Ofisi yake kwa kutoa huduma nzuri kwa Watumishi na Wananchi wenye uhitaji wa huduma na kuifanya Ofisi hiyo kuwa kimbilio wakati wote kwa huduma za Kiutumishi.

Kaimu Katibu Mkuu huyo ametoa pongezi hizo hivi karibuni wakati alipowasili katika Ofisi hizo zilizopo Mtumba, Dodoma kutekeleza majukumu yake ya kila siku na kukutana na watumishi wake waliokuwa wakitoa huduma katika eneo la mapokezi.

"Hakikisheni mnatoa maelezo sahihi na huduma bora na haraka kwa kila Mtumishi au Mwananchi anayekuja kupata huduma katika Ofisi hii, uharaka na ufanisi wetu, utawapa wateja nafasi ya kuendelea na shughuli nyingine za kujenga uchumi wa nchi" amesema Bw.

Vilevile, ameongeza kuwa, Wiki hii ni muhimu sana katika usimamizi wa utoaji huduma kwa umma kwa kuwa inasaidia kuimarisha uhusiano baina ya Ofisi na wateja, lakini zaidi kuwafikia Watumishi na Wananchi kwa njia mbalimbali na kutatua shida zao kwa ufanisi na haraka.

Aidha, Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Usimamizi wa rasilimaliwatu, Ofisi ya Rais, UTUMISHI Bw. Mussa Magufuli amebainisha kuwa kupitia Wiki ya Huduma kwa Wateja, Ofisi itahakikisha inakutana na wateja ili kupata maoni, mapendekezo ya kuboresha huduma na kutatua changamoto mbalimbali za kiutumishi zinazowakabili watumishi na wananchi.

Wiki ya Huduma kwa Wateja huadhimishwa kila mwaka katika wiki ya kwanza ya Oktoba ambapo mwaka huu, wiki hii imeanza Oktoba 7 na itahitimishwa Oktoba 11, 2024.





*Kaimu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Bw. Xavier Daudi akizungumza na baadhi ya watumishi wake waliokuwa wakitoa huduma katika eneo la mapokezi katika Ofisi zilizopo Mtumba, Dodoma*

# 8 NAIBU WAZIRI SANGU AITAKA SERIKALI KUWAUZA VIJANA WABUNIFU WA TEHAMA



*na Lusungu Helela - Dodoma*

Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Deus Sangu ameitaka Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) kushiriki kwenye Maonesha mbalimbali ya Ubunifu ili kuonesha uzuri wa mifumo iliyobuniwa pamoja na umahiri wa vijana walioandaliwa na Taasisi hiyo ili vijana hao waweze kupata soko kwenye Sekta Binafsi.

Ametoa kauli hiyo hivi karibuni wakati akifunga mafunzo kwa vitendo kwa Wanafunzi 65 wa Vyuo Vikuu mbalimbali yaliyofanyika kwa kipindi cha muda wa wiki kumi katika Kituo cha Ubunifu na Utafiti cha eGA kilichopo jijini Dodoma.

Ameitaka eGA kutekeleza program hiyo ya kukuza ubunifu katika TEHAMA kwa wanafunzi wa Elimu ya juu kimkakati kwa kuwakutanisha vijana hao na Waajiri ambao ni sekta binafsi.

Kufuatia hatua hiyo Mhe.Sangu ameitaka eGA kuimarisha ushirikiano zaidi na Sekta binafsi ili vijana wanaoandaliwa na Taasisi hiyo waweze kukidhi hitaji la soko la ndani na nje ya nchi katika eneo la Tehama bunifu.

"Nimefarijika kusikia Benki ya NMB pamoja na Kampuni ya Vodacom ni miongoni mwa washirika wenu ambao mnashirikiana nao kwa kuwaeleza mahitaji ya soko na hivyo kuisaidia jinsi ya kuwapika vijana ili waendane na hitaji la soko", amesema Mhe. Sangu.

Ameongeza kuwa "Nimeambiwa mwaka jana Benki ya NMB ilichukua jumla ya vijana nane mliowaandaa, hii ni habari njema sana kwetu kama Serikali".

Katika hatua nyingine, Mhe.Sangu ameitaka eGA kuandaa kanzidata kwa vijana wote wanaopata mafunzo kwa vitendo katika Kituo hicho badala ya kuwaacha tu bila ya kuwa na taarifa zao.

Amesema ili kuhakikisha TEHAMA inatoa matokeo tarajiwa kwa Uchumi wa nchi ya Tanzania vijana hao wanadiwe kwa bunifu zao wanazofanya Ili kuweza kuwashawishi waajiri.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao, Mhandisi. Benedict Ndomba amesema kuwa Kituo hicho kimekuwa kikifanya tafiti katika maeneo yote ya TEHAMA kwani tafiti hizo na bunifu zinaiweka nchi katika nafasi nzuri ya kushindana kwenye Uchumi wa kidijitali na Mataifa mengine.

Naye, Jane Claud ambaye ni mwanafunzi aliyepata mafunzo kwa vitendo katika Kituo hicho licha ya kushukuru kwa kupata fursa hiyo ameiomba Serikali kuharakisha ujenzi wa kituo kikubwa ili kuendana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia yanatokea duniani.




*Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe.Deus Sangi akizungumza wakati akifunga mafunzo kwa vitendo kwa Wanafunzi 65 wa Vyuo Vikuu mbalimbali yaliyofanyika kwa kipindi cha muda wa wiki kumi katika Kituo cha Ubunifu na Utafiti cha eGA kilichopo jijini Dodoma*



*Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe.Deus Sangu akiwa kwenye picha pamoja na Wanafunzi 65 wa Vyuo Vikuu mbalimbali wakati akifunga mafunzo kwa vitendo yaliyofanyika kwa kipindi cha muda wa wiki kumi katika Kituo cha Ubunifu na Utafiti cha eGA kilichopo jijini Dodoma*



*Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe.Deus Sangu ( kulia ) akiwa na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao Eng. Benedict Ndomba pamoja na timu ya Menejimenti mara baada ya kuwasili kwa ajili yq kufunga mafunzo kwa vitendo kwa Wanafunzi 65 wa Vyuo Vikuu mbalimbali yaliyofanyika kwa kipindi cha muda wa wiki kumi katika Kituo cha Ubunifu na Utafiti cha eGA kilichopo jijini Dodoma*



*Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe.Deus Sangu akizungumza na Mkurugenzi mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao Eng. Benedict Ndomba wakati wa ufungaji wa mafunzo kwa vitendo yaliyofanyika kwa kipindi cha muda wa wiki kumi katika Kituo cha Ubunifu na Utafiti cha eGA kilichopo jijini Dodoma*




*Mkurugenzi mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao Eng. Benedict Ndomba akizungumza kabla ya kumkaribisha Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe.Deus Sanga kwa ajili ta kufunga mafunzo kwa vitendo kwa Wanafunzi 65 wa Vyuo Vikuu mbalimbali yaliyofanyika kwa kipindi cha muda wa wiki kumi katika Kituo cha Ubunifu na Utafiti cha eGA kilichopo jijini Dodoma*



# 9 MHE. SIMBACHAWENE AFANYA MAZUNGUMZO NA RAIS DKT. MWINYI



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. George Simbachawene hivi karibuni amemtembelea na kufanya mazungumzo na Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi nyumbani kwake Osterbay Jijini Dar es Salaam.

Katika mazungumzo hayo Mhe. Simbachawene amemueleza Mhe. Dkt. Mwinyi kuwa Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amemuelekeza kumfikishia salaam kwa familia ya Hayati Ali Hassan Mwinyi na kuahidi kuendelea kuwa pamoja na familia hiyo kwa kuwa ni wajibu wa Ofisi yake kutunza wenza wa Viongozi wa Kitaifa na yeye yuko tayari kuendelea kutekeleza wajibu huo.

Mhe. Simbacahwene aliongeza kuwa anafanya ziara ya kuwajulia hali Wenza wa Viongozi hao ili kufahamu changamoto zinazowakabili na kuzitafutia ufumbuzi.

Aidha, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi ameshukuru kwa ujio huo na kupongeza utaratibu uliopo wa kuwatembelea wanafamilia na kuwapa faraja.




*Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Deus Sangu*
*...ara*
*...adi*
*...i za*
*... ya*
*...ora*

# 10 KATIBU MKUU-UTUMISHI ATAKA WAKURUGENZI WA UTAWALA NA USIMAMIZI WA RASILIMALIWATU KUIMARISHA MFUMO WA UTOAJI HAKI

*Na Veronica Mwafisi - Dodoma*

Kaimu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Bw. Xavier Daudi amewataka Wakurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu wa Wizara pamoja na Waratibu wa Jinsia Ngazi ya Wizara kuweka mbinu za kuimarisha mfumo wa utoaji haki, kudhibiti uonevu, dhuluma, unyanyasaji na unyonyaji wa kijinsia pamoja na kuingiza masuala ya jinsia katika Mipango, Mikakati na Programu ya Wizara zao ili kuleta maendeleo endelevu.

Bw. Daudi amesema hayo hivi karibuni wakati akifungua semina elekezi ya Mwongozo wa Jinsia kwa Wakurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu wa Wizara pamoja na Waratibu wa Jinsia Ngazi ya Wizara katika Ukumbi wa Kambarage, Wizara ya Fedha, jijini Dodoma.

Amesema kumekuwepo na viashiria na matukio mbalimbali ya kutowatendea haki baadhi ya watumishi kutokupata stahiki zao kwa wakati, kutopewa nafasi za kujiendeleza, kukataliwa uhamisho, kutopewa likizo na nauli ya likizo, madai ya muda mrefu kwa watumishi, na unyanyasaji na dhuluma za kijinsia mahali pa kazi, udhalilishaji na uonevu ambao kwa kiasi kikubwa umewafedhehesha watumishi na kutweza utu wao.

"Baadhi ya watumishi wamekuwa wakinyanyasika katika maeneo yenu ya kazi kwa kunyimwa haki zao za msingi, niwasisitize kusimamia jambo hili mara moja kwani mwisho wake watumishi hao watashindwa kufanya kazi zao kwa ukamilifu na kurudisha nyuma maendeleo ya taifa letu," Bw. Daudi amesisitiza.

Amesema ujumuishwaji wa masuala ya jinsia ni muhimu sana maana ni chachu na huleta



Amesema Serikali imeendelea na jitihada za kuimarisha Usawa wa Kijinsia katika Utumishi wa Umma ikiwa ni pamoja kuweka mazingira wezeshi yanayozingatia mahitaji ya kijinsia na hatua za makusudi (affirmative actions) ya kuongeza ushiriki wa wanawake katika nafasi na majukumu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kushiriki katika nafasi za uongozi na maamuzi ili kuzifikia fursa na kujenga usawa kati ya wanawake na wanaume na kuwezesha utekelezaji wa lengo namba tano (5) la Malengo Endelevu ya Mwaka 2030 kufikia Usawa wa Kijinsia kwa asilimia 50.

Bw. Daudi ameishukuru Taasisi ya UONGOZI kwa kuendelea kutafsiri ndoto za Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambapo kwa nyakati tofauti wameandaa programu za Uongozi kwa Wanawake awamu kwa awamu na kuwezesha kufanyika kwa Semina elekezi juu ya mwongozo wa ujumuishwaji wa Jinsia katika Utumishi wa Umma kwa Ngazi ya Wizara.

Semina hiyo ya siku mbili imeratibiwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kushirikiana na Taasisi ya UONGOZI.




*Kaimu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-UTUMISHI, Bw. Xavier Daudi akiwa katika picha ya pamoja na Wakurugenzi kutoka katika ofisi hiyo mara baada ya kufungua semina elekezi ya Mwongozo wa Jinsia katika Utumishi wa Umma iliyofanyika jijini Dodoma.*



*Wakurugenzi wa Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu kutoka Wizara zote na Waratibu wa Ujumuishwaji Jinsia ngazi ya Wizara wakimsikiliza Kaimu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-UTUMISHI, Bw. Xavier Daudi (hayupo pichani) wakati akizungumza nao kwenye semina elekezi ya Mwongozo wa Jinsia katika Utumishi wa Umma.*



*Wakurugenzi wa Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu kutoka katika Wizara mbalimbali wakifanya mazoezi kwa vitendo kuhusu Ujumishwaji wa Jinsia wakati wa semina elekezi ya Mwongozo wa Jinsia katika Utumishi wa Umma iliyofanyika jijini Dodoma.*



*Kaimu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-UTUMISHI, Bw. Xavier Daudi akizungumza na Wakurugenzi wa Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu kutoka Wizara zote na Waratibu wa Ujumuishwaji Jinsia ngazi ya Wizara wakati akifungua semina elekezi ya Mwongozo wa Jinsia katika Utumishi wa Umma.*



# 11 MHE. SIMBACHAWENE AMTEMBELEA MAMA SITTI MWINYI



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. George Simbachawene amemtembelea Mama Sitti Mwinyi (Mke wa Hayati Rais Mstaafu Ali Hassan Mwinyi) nyumbani kwake Mikocheni Jijini Dar es Salaam hivi karibuni.

"Rais, amenielekeza kuwafikishia salaam zake na amesema yuko pamoja nanyi na ndio mana amenituma kufika hapa nyumbani na kuwajulia hali, kusikiliza changamoto zilizopo na kuzitafutia ufumbuzi" amesema Mhe. Simbachawene.

Mhe. Simbachawene amesema Rais Mhe. Dkt. Samia anathamini sana mchango wa Viongozi Wakuu wa Kitaifa waliomtangulia na ataendelea kusimamia na kutunza familia hizo kwa mujibu wa Katiba na Sheria.

Aidha, Mama Sitti amemshukuru Mhe. Simbachawene kwa kupata nafasi ya kumtembelea na kumjulia hali na amempongeza Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuijali familia yake wakati wote bila kuchoka na amemuombea kwa Mungu aendelee kutumia hekima na busara katika kuiongoza Tanzania.

## 12 MHE. SANGU AHIMIZA MAFUNZO YA UONGOZI KWA BODI MBALIMBALI




Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Deus Sangu ameitaka Taasisi ya Uongozi kuweka kipaumbele kwenye mafunzo yanayohusisha wajumbe wa bodi mbalimbali za Mashirika ya Umma ili kujenga uelewa mpana wa masuala ya kiuongozi ili wanapofanya uamuzi wowote wazingatie maslahi mapana ya Taifa.

Mhe. Sangu ametoa rai hiyo hivi karibuni jijini Dar es salaam wakati alipofanya ziara ya kujifunza namna taasisi hiyo inavyofanya kazi na kuhimiza uwajibikaji kwa watumishi.

“Nimefarijika sana kusikia kuwa Taasisi ya Uongozi inatoa mafunzo mahususi ya kuwajengea uwezo wa kiutendaji viongozi mbalimbali ndani na nje ya Tanzania ikiwa pia ni sehemu ya utekelezaji wa jitihada za kuimarisha utawala bora”.

Ameongeza kuwa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan anafanya jitihada za kujenga nchi yetu katika nyanja mbalimbali, hivyo hatuna budi kumuunga mkono kwa kufanya mafunzo ambayo yanaweza kuwafanya viongozi mbalimbali kuwa wazalendo na wenye kiu ya kuona taifa linapata maendeleo.

Vile vile, amesisitiza watumishi wa Taasisi hiyo kuendelea na mshikamano katika kutekeleza majukumu yao kwa kuwa jukumu la kutoa mafunzo kwa Viongozi ni kubwa na linahitaji mshikamano.

Mhe. Sangu amefanya ziara katika Taasisi ya Uongozi kwa kwa lengo la kujifunza kuhusu majukumu ya Taasisi hiyo ambayo ipo chini ya Ofisi anayoiongoza.



## 13 MHE. SIMBACHAWENE ATETA NA RAIS KIKWETE



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. George Simbachawene leo amemtembelea na kufanya mazungumzo na Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne Mhe. Dkt. Jakaya M. Kikwete nyumbani kwake Kawe Jijini Dar es Salaam.

Katika mazungumzo hayo, Mhe. Simbachawene amefikisha salaam za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ameahidi kuendelea kuwa pamoja na Viongozi Wakuu Wastaafu wa Kitaifa kwa maendeleo ya taifa.

Mhe. Simbachawene amesema Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ina jukumu la kutunza Viongozi Wakuu Wastaafu Kitaifa na Wenza wao, hivyo yuko tayari kuendelea kutekeleza jukumu hilo alilopewa na Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa ufanisi.

Hali kadhalika, Mhe. Dkt. Kikwete amemshukuru Mhe. Simbachawene kwa ujio huo na kupongeza utaratibu uliopo wa kuwatembelea Wiongozi Wakuu Wastaafu wa Kitaifa kwa kuwa unawapa faraja, unaonesha thamani na mchango wao kwa maendeleo ya taifa



# 14 RAIS MHE. DKT. SAMIA ACHANGIA MILIONI 50 KANISA LA MENNONITE

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. George Simbachawene ametoa rai kwa waamini wa Kanisa la Mennonite Tanzania ya kuendelea kulinda umoja, amani, uhuru, mshikamano na ustawi wa watanzania kwa maendeleo ya Taifa la Tanzania.

Mhe. Simbachawene ametoa rai hiyo wakati alipomwakilisha Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye harambee ya kuchangia ujenzi wa Kituo cha Elimu Mkamba cha Kanisa la Mennonite Tanzania, iliyofanyika katika kanisa la Mennonite Dayosisi ya Mashariki, Jijini Dar es salaam.

"Rais wetu Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, anatambua umuhimu wa elimu kwa watanzania, hivyo anachangia milioni 50 ikiwa ni jitihada za kuhakikisha kituo kinajengwa haraka ili watoto wetu waweze kupata elimu ya dunia na ya kiroho, na mimi nilitamani kuchangia milioni 2.5 lakini kwa mahubiri ya Baba Askofu Gabriel Magwega, Askofu wa Kanisa la Mennonite Tanzania, Dayosisi ya Mashariki yamenigusa kutoa zaidi, sasa nitatoa sadaka milioni 5 ili kujenga kituo hiki cha kuandaa rasilimaliwatu" Mhe. Simbachawene.

Mhe. Simbachawene aliongeza kuwa rasilimawatu ikiandaliwa vizuri na kupata elimu bora, nchi itapata viongozi wenye hofu ya Mungu na watakuwa na uwezo wa kuongoza nchi kwa kuzingatia maadili mema, hivyo kuleta maendeleo ya haraka kwa taifa na wananchi kwa jumla.

Aidha, aliongeza kuwa Serikali inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan iko tayari kushirikiana na Kanisa katika kuondoa maadui watatu yaani ujinga, maradhi na umaskini. Kwa hiyo ujenzi wa Kituo hicho cha Elimu cha Mkamba ni msingi wa kupambana na maadui hao.

Awali, Baba Askofu Nelson Kisare, Askofu Mkuu wa Kanisa la Mennonite Tanzania alisema kuwa Serikali imeridhia Malengo 17 ya Umoja wa Mataifa kuhusu Elimu (SDG) ambapo katika malengo hayo lengo namba 4 linahusu elimu hususani Elimu Jumuishi, kwa mantiki hiyo Kanisa la Mennonite Tanzania linaunga mkono Serikali katika jitihada za kutekeleza malengo hayo kwa kuandaa mazingira bora ya kutoa elimu kwa watanzania.

Vilevile, aliongeza kuwa Kanisa litaendelea kushirikiana na Serikali katika utoaji wa elimu bora kwa wasichana na wavulana ili kuunga mkono jitihada za kuondoa ujinga, maradhi na umaskini. Pia, kanisa litahakikisha katika shule hiyo linatoa vijana wa kitanzania waliolelewa katika misingi ya neno la Mungu, wenye kumcha Mungu na wenye hofu ya Mungu ndani ya mioyo yao.

"Waziri, Mhe. Simbachawene tunaomba utufikishie salaam zetu za shukurani kwa Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kupokea barua yetu, kukubali mwaliko na kukutuma wewe kuja kumuwakilisha, jambo hili ni kubwa sana na sisi tutaendelea kumuombea kwa Mungu ili aendelee kuongoza nchi hii kwa amani, furaha na upendo daima" alisema Baba Askofu Kisare.



# 15 MHE. SIMBACHAWENE AKUTANA NA WENZA WA VIONGOZI WA KITAIFA



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. George Simbachawene hivi karibuni kwa nyakati tofauti amewatembelea na kufanya mazungumzo Mama Anna Mkapa na Mama Janeth Magufuli katika makazi yao Osterbay Jijini Dar es Salaam.

Katika mazungumzo yake na wenza wa viongozi hao, Mhe. Simbachawene ameahidi kuwaelekeza watendaji katika ofisi yake, kushughulikia changamoto zinazojitokeza na kuwafanya wenza wa viongozi hao kuendelee kuishi kwa amani na usalama.

Aidha, Mama Mkapa amemshukuru Mhe. Simbachawene kwa kupata nafasi ya kumtembelea, kumjulia hali na kusikiliza changamoto alizonazo na kuzitafutia ufumbuzi.

Vilevile Mama Janeth Magufuli amempongeza Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuijali familia yake na kuwatunza wakati wote bila kuchoka na amemuombea kwa Mungu aendelee kuiongoza vyema Tanzania.



# 16 MHE. SANGU AWATAKA WATUMISHI WA TASAF KUWA WABUNIFU



Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Deus Sangu ametoa rai kwa watumishi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kuwa wabunifu ili fedha zinazopelekwa kwa wananchi zisiende kama msaada isipokuwa ziende kwa mantiki ya kuwainua na kuwatoa kwenye wimbi la umaskini.

Mhe. Sangu ametoa rai hiyo hivi karibuni jijini Dar es salaam wakati alipofanya ziara ya kujifunza namna taasisi hiyo inavyofanya kazi na kuhimiza uwajibikaji kwa watumishi.

Amesema, mpango wa kunusuru kaya maskini ni muhimu sana kwa wananchi, hivyo alielekeza menejimenti kuendelea kufikiri na kufungamanisha programu za kunusuru kaya maskini na programu nyingine ili kuwatoa walengwa kwenye umaskini.

Aidha, aliongeza kuwa Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan anaendelea kutafuta fedha na kuzipeleka kwa walengwa wengi zaidi, hivyo jitihada za kunusuru kaya maskini zinatakiwa kuimarishwa zaidi na watendaji.

Aidha, Mhe. Sangu ameomba menejimenti na watumishi wa TASAF kumpa ushirikiano hasa anapotaka taarifa za mfuko ili kujibu hoja na kutoa ufafanuzi wa masuala mbalimbali ya TASAF kwa Waheshimiwa Wabunge.

“Mimi milango iko wazi wakati wote, iwapo mtapata changamoto yoyote inayohitaji mawazo au ushauri wangu, niko tayari kuwasaidia kwa kuwa ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu yangu” alisisitiza Mhe. Sangu.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF Bw. Shedrack Mziray alisema malipo ya ruzuku kwa walengwa hufanywa kwa kutoa fedha taslimu kwa kutumia kamati ya usimamizi wa shughuli za mipango kwa jamii chini ya usimamizi wa ngazi ya utekelezaji wa mpango (Halmashauri) na njia ya pili ni ya kieleketroni.

Bw. Mziray ameongeza kuwa njia zote ni muhimu kwa walengwa ingawa njia ya kieletroni ni muhimu zaidi kwa kuwa inarahisisha utoaji wa ruzuku kwa walengwa ingawa kuna changomoto mbalimbali zinazowakabili wanufaika.

Alibainisha kuwa mwaka 2023 TASAF ilifanya tathmini na kubaini kaya za walengwa 394,305 zimeimarika kiuchumi na kukidhi vigezo vya kuhitimu na hivyo hazitaendelea kupewa ruzuku kama ilivyokuwa hapo awali.

Mhe. Sangu amefanya ziara kwa lengo la kujifunza kuhusu majukumu ya Mfuko huo ambao upo chini ya Ofisi anayoiongoza.

## WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA, MHE. GEORGE SIMBACHAWENE WAKATI AKIFUNGA MICHEZO YA SHIMIWI 2024 MKOANI MOROGORO

















**IMETOLEWA NA**

Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa
Umma na Utawala Bora

**Oktoba, 2024**